# KIELEKEZI SAHIHI CHA KARATASI YA 3
# 102/3
# FASIHI 2026

KIELEKEZI SAHIHI

## KIELEKEZI 1

### SEHEMU YA A: L A Z I M A

### FASIHI SIMULIZI

***Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali***

Mwanangu kumbuka kuwa nidhamu ni msingi wa maisha yenye mafanikio. Utukutu na ukaidi vinaweza kukupeleka katika njia mbaya na zikufanye kukosa **kufua dafu** katika mustakabali wako. Ni muhimu uwaheshimu wazazi, walimu na watu wengine wakubwa kwani ushauri wao utakujenga na kukuelekeza vyema. *Fom* marafiki wenye maadili mema na ujiepushe na makundi mabaya. **Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu**. Hivyo ukikataa mawaidha mema mapema utapata shida kubwa maishani upate maangamizi yakikupokea kwa mikono miwili.

a) Tambua utanzu wa utungo uliousoma. (alama 2)

b) Kando na mbinu zilizopigiwa mstari, eleza mbinu nyingine zozote mbili za kimtindo katika kifungu. (alama 2)

c) Eleza njia nyingine tano ambapo vipera vilivyopigiwa mstari vinaweza kutumika. (alama 5)

d) Fafanua changamoto zinazokumba kuendelea kwa fasihi simulizi. (alama 5)

e) Eleza jinsi ya kuvifanya vipera vilivyokolezwa visipotee katika jamii ya kisasa (alama 6)

## SEHEMU B: RIWAYA

**Clara Momanyi:** ***Nguu za Jadi***

*Jibu swali la 2 au la 3*

**2. "Maisha ni kama kidau kinachoelea baharini. Ni sawa na upepo wa maleleji. Huna hakika na maisha. Lakini ikiwa yatakubwaga, ni vizuri kuanguka kingalingali."**

i. Eleza Muktadha wa dondoo. (alama 4)

ii. Mbinu za lugha zinazojitokeza katika dondoo. (alama 2)

iii. Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha jinsi mwanamke alivyoumbuliwa katika riwaya ya Nguu za Jadi. (alama 14)

**3. "Ebo! Serikali unayosema ni nani hasa? Serikali ni sisi wananchi, kaka. Hata huyo lesulia unajuaje atakuwa mtemi wetu tena? Umeishi ndani ya kivuli cha Lesulia kiasi cha kwamba hujui uchaguzi unabisha? Umo ndotoni wewe! Aliye juu msubiri chini, kaka. Wavyele hawakukosea waliposema ulichokiacha pwani kakingoje ufuoni. Kunifuta kazi si suluhisho la matatizo yenu. Afisi hii umeijaza wakule watupu. Hata matarishi wote umewaleta wewe. Nina hakika hata yule msichana anatoka kwenu. Si mtasalia nyie watupu mkiongea lafudhi yenu hapa? Hata yule topasi najua utamfuta kazi tu maana twajua atokako…Kama unadhani ukabila ni chakula, basi nakuambia hivi; kapike ule na wa kwenu!"**

a) Changanua mbinu za kimtindo zinazojitokeza kwenye kifungu. (alama 5)

b) Bainisha maudhui mawili yanayojitokeza kwenye kifungu. (alama 2)

c) Fafanua jinsi suala la ufisadi linavyobainishwa kwa kurejelea riwaya nzima.(al.12)

## SEHEMU B: TAMTHLIA

**Timothy M. Arege:** *Bembea ya Maisha*

**4. "Hayo ni ya kale…na ya kale hayanuki. Wengi hawafuati tena mila hizo. Walimwengu sasa wanavaa sare moja."**

i. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

ii. Eleza umuhimu wa msemaji wa maneno haya. (alama 6)

iii. Eleza maudhui ya mila na utamaduni jinsi inavyojitokeza katika tamthlia ya Bembea ya Maisha. (alama 10)

KIELEKEZI SAHIHI

**5. “Lakini nimeona ukatili wa baba ulivyokulemaza. Zamani watu walikuwa wakisema kuwa maneno hayadhuru lakini tazama yalivyokudhuru. Tazama matokeo ya vipigo vyake. Naye neema ameolewa na bahili mkubwa asiyejua maana ya familia. Hatuoni kama watu. Ni yeye na lake tu.”**

i. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
ii. Maudhui yanayojitokeza katika dondoo. (alama 3)
iii. Eleza sifa za msemaji wa maneno haya Sifa za Asna. (alama 4)
iv. Thibitisha kuwa Neema anakumbana na ubahili kutoka kwa Bunju katika ndoa yake. (alama 9)

## SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

**D.W Lutomia na Phibian Muthama:** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

**Jibu swali la 6 au la 7**

**6. “Hatuwezi kuruhusu jambo lolote linaloelekea kuivunja familia ya Belo. Wale miongoni mwetu wasiobahatika kupata kazi huko migodini wana wajibu wa kuhakikisha kuwa familia yetu haisambaratiki. Kesho asubuhi, wengine wetu wataandamana nawe mpaka Habelo ili tukusaidie kumzika mtoto. Utabeba maiti ya mtoto huyo mgongoni mwako, kama ulivyoibeba kuileta hapa. Nimesema!”**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Fafanua maudhui matano yanayojitokeza katika dndoo hili. (alama 5)
c) Eleza toni inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 1)
d) Mwanamke amesawiriwa kama kiumbe dhaifu katika jamii. Thibitisha kwa kurejelea hadithi ya Sabina. (alama 10)

**7. *Msiba wa Kujitakia* –** D.W. Lutomia

**“Kongole kwa `ushindi` wako, ingawa ushindi huo huenda usione jua!Kaka wewe ni shujaa. Kisa chako ni mfano tajika wa jinsi ndoto na nia za vijana zimebanwa, zikafinywa na kuzimwa. Mambo yangalifanyika kinyume, basi Matopeni ingalikuwa na hadhi tofauti.**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 5)
b) Eleza umuhimu wa msemaji (alama 5)
c) Kisa chako ni mfano tajika wa jinsi ndoto na nia za vijana zimebanwa, eleza kauli hii. (alama 10)

KULEKEZI SAHIHI

## SEHEMU YA D: USHAIRI

**Jibu swali la 8 au 9**

***9. soma shairi kisha uyajibu maswali***

VITATURUDIA

Kwa sisi wanaohabibu
Kwa wale wengi, wengi mno, wanaosulubu
Kwa wale wenye nyoyo zilizojaa ghadhabu
Na kwetu sisi warithi tulionyang'anywa
Tuloungana kama bawabu

Kwetu sisi sote…
Vyote vitakuja
Vitaturudia pamoja
Vitakuwa vyetu tena siku moja

Mashamba ya wahenga wetu
Mabonde na miteremko yetu
Milima inayovutia nadhari zetu
Vyote vitakuja
Vitakuwa vyetu tena siku moja.
Ardhi yenye manukato ya rutuba
Nyasi zilosimama wima kwa kushiba
Misitu ilosongana kwa mengi mahaba
Vyote vitakuja
Vitakuwa vyetu tena pamoja

Mito kwa furaha ikimiminika
Maziwa yaliyokitwa yakakitika
Na bahari zipovukavyo katika zake haraka
Vyote vitakuja
Vitakuwa vyetu tena siku moja.

Kwa wale wanaoweza kungojea
Kwa wale wanaoweza kuvumilia
Kwa wale wenye majaraha, waloumia
Walothamini usiku wa baridi

Uhuru kuupigania
Kuliko mwezi na nyota kuzifurahia

KILELEKEZI SAHIHI

Hali ni watumwa, watu wa kutumikia
Kwa hao wote
Vyote vitakuja
Vitawarudia pamoja
Vitakuwa vyao tena siku moja.

(Alamin Mazrui, Chembe cha moyo)

a) Eleza shairi hili ni la aina gani. (alama 2)
b) Eleza ujumbe wa mshairi katika shairi hili. (alama 4)
c) Eleza matumizi ya mbinu ya tashihisi katika utungo. (alama2)
d) Thibitisha kuwa utungo fulani ni shairi huru. (alama 3)
e) Changanua muundo wa shairi hili (alama 4)
f) Eleza aina mbili za taswira zinazojitokeza katika shairi (alama 2)
a) Jadili mbinu ya urudiaji kama ilivyotumika katika shairi. (alama 3)

***9. soma shairi kisha uyajibu maswali***

Ilipoanza safari, ilianza kwa dhiki
Tulisihka kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

Njaa ikawa thabiti, na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati, tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti, dhila na mingi mikiki
tulijizatiti

Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari, juhudi iliyobaki
tulijizatiti

Ile ilikuwa ndoto, mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto, sahala 'mekuwa dhiki
Wagombania kipato, utashi haukatiki
Na kutabakari

Msafara ukasita, kwenye mlima wa haki

KIELELEZI SAHIHI

Kijasho kinatuita, mlima haupandiki
Basi sote 'kajipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina

Tukiwa migongo wazi, tukainama kwa shaki
Takawa'chia ukwezi, kialeni wadiriki
Wakapanda bila kazi, kuteremsha miliki
Wakaitapia

Wakafikia makazi, ya pumbao na ashiki
Huko wakajibarizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma ulomiliki
Mbele ya safari

Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema mate, kwa umati halaiki
Imezima nia yote, kiza hakitakasiki,
Mbele ya safari.

***Said A. Mohamed.***

a) Eleza safari inayorejelewa katika shairi hili. (alama 2)
b) **Onyesha kinaya** cha safari inazungumziwa. (alama 6)
c) Taja na **ueleze bahari mbili za shairi** hili ukizingatia: (alama 4)
   I. Mizani
   II. Vina
d) Andika ubeti wa saba kwa **lugha ya nathari** (alama 4)
e) Eleza **umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi** zilizotumiwa katika ubeti wa sita. (alama 4 )

KIELEKEZI SAHIHI

# KIELEKEZI 2

## SEHEMU A: TAMTHLIA

**Timothy M. Arege:** *Bembea ya Maisha*

**1. "Wewe si kama wale wanawake ambao hawana kazi wala bazi. Tangu hapo nimekupa ikibali kuiinua familia yako kwa huo mshahara wako. Sijateta wala kununa."**

i. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
ii. Eleza sifa za mzungumziwa wa maneno haya. (alama 6)
iii. Huku ukirejelea tamthlia ya Bembea ya Maisha, eleza jinsi Bunju na Neema wanavyoendeleza maudhui ya kazi. (alama 10)

## SEHEMU B: RIWAYA

**Clara Momanyi:** *Nguu za Jadi*

*Jibu swali la 2 au la 3*

**2. "Ole wako wewe mwanaume uishiye leo. Unayechakura mapipa ili kuizima njaa. Uliikosea nini jamii ili usalie kuwa ombaomba? Umevaa koti kuukuu na umesalia kuwa nyuma kama koti hilo mwenetu. Yu wapi baba aliyekutelekeza? I wapi jamii isiyothamini elimu na utu wako? Jamii ilimshika mkono mtoto wa kike. Ikapiga mbio na mtoto wa kike. Ikasahau kwamba hata wewe unastahili kushikwa mkono. Lazima tujirudi, tuone ni wapi tulipoanza kupotea njia. Lazima <u>tuokoe kizazi hiki kinachopotea nyikani bila matumaini.</u> Ole wako Matuo, utashika mti gani?"**

i. Changanua mtindo katika kifungu. (alama 6)
ii. Eleza maudhui yanayoendelezwa na kizazi hiki kinachopotea bila matumaini kwa mujibu wa mandhari ya dondoo . (alama 8)
iii. Eleza jinsi Sagilu anavyoendeleza suala la maudhui ya ufisadi ukirejelea riwaya yote. (alama 6)

**3. "Na huyu ndiye aliyebeba vishawishi na tamaa zote za ulimwengu. Lakini mbona Mwenyezi Mungu hakuumba aliye mzuri jamani?"**

i. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
ii. Eleza toni inayojitokeza katika dondoo. (alama 1)
iii. Kwa hoja kumi, fafanua maudhui ya tamaa kama yalivyotumika katika riwaya ya Nguu za Jadi. (alama 15)

KIELEKEZI SAHIHI

## SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

**D.W Lutomia na Phibian Muthama:** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4. "Hata niliporudi mezani kupumua na angalau niteremshe kidogo, akanijia binti fulani akaniomba tucheze. Mwenyewe amejiremba kwa kila aina ya maleba, utafikiria anaingia jukwaani kuigiza drama."**

a) Eleza muktadha wa maneno katika dondoo hili. (alama 4)

b) Fafanua umuhimu wa msemaji wa dondoo hili. (alama 6)

c) Umaskini ni kikwazo kikubwa katika kudumisha ndoa. Eleza kwa mujibu wa hadithi ya *Harubu ya Maisha.* (alama 10)

**5. "Kisa chako ni mfano tajika wa jinsi ndoto na nia za vijana zimebanwa, zikafinywa na kuzimwa. Mambo yangalifanyika kinyume, basi matopeni ingalikuwa na hadhi tofauti. Kaka, ndoto haifi ila vizingiti haviishi daima; kulimbikiziwa viongozi, udikteta, ukoloni mamboleo…yataje yote…ila kesho…kesho…kesho yote haya yatakuwa marehemu na uhai wao utakuwa katika mabuku ya historia. Ndugu, utavuma kesho, na hiyo kesho viongozi watachaguliwa. Uchaguzi huo utakuwa huru na wa haki. Mizani ya ubora wa kiongozi haitakuwa kabila lako, ukoo wako, familia yako, nani unayemjua, una hela ngapi…kesho hoja zitakuwa msingi wa kupimia ubora wa wawaniaji uongozi."**

a) Changanua mtindo katika kifungu hiki. (alama 5)

b) Eleza maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili. (alama 6)

c) Kutamani ni huhitaji ambao umetawaliwa na tamaa katika hadithi ya **'Nilitamani.'** kulingana na '**Phibbian Muthama'** Pambanua haya kulingana na hadithi husika. (alama 10)

KIELELEZI SAHIHI

**SEHEMU YA D: USHAIRI.**
**Jibu swali la 6 au 7**

**6.** Uwapo ulimwenguni, mijini na vijijini,
Unaishi na wengini, marafiki na jirani,
Yafaa kutathmini, uwatie kwa mizani,
Yupi aitwe mwandani, wa kuepuka n'nani

Kwanza kunaye fatani, apendaye kufitini,
Huchonganisha insani, kwa maneno ya kinywani,
Ukiyatia moyoni, wakosana na wendani,
Usimfanye mwandani, ajakusoza dhikini.

Kuna na msengenyaji, na shushushu mdomoni,
Hakikisha kwako haji, akazusha **tafrani,**
Huyu hayakosi mauji, usimwalike nyumbani,
Usimfanye mwandani, akusoza hatarini.

Mwepuke na mzinifu, apendaye ubatani,
Yake sio timilifu, ni tabia yenye guni,
Matendo yake dhaifu, watu hawamthamini,
Usimfanye mwandani, akusoza hatarani.

Umwonapo na jambazi, **anahanja** mitaani,
Ni bingwa wa **kubazazi**, akurenge akilini,
Mwisho wake ni mauzi, akutosa matopeni,
Usimfanye mwandani, akusoza hatarini.

Mtambue na tapeli, ni ayari wa kuhini,
Atakuchapa kauli, za utamu kama nini,
Na kukuteka akili, hadi uweze mwamini,
Usimfanye mwandani, akusoza hatarini.

Vitu aweza nyang'anya, ubaki na laitani,
Juku hela azisanya, kwa hila huyu kaini,
Akishaupata mwanya, utamlilia Manani,
Usimfanye mwandani, akusoza hatarini.

Halafu yupo na mwongo, sithubutu kumwamini,
Mambo yake yana ongo, hayafani asilani,

KIELIKEZI SAHIHI

Huapa kuwa ni mrongo, kikwangalia machoni,
Usimfanye mwandani, akusoza hatarini.
(*Mtunzi K. W. Wamitila)*

**Maswali**

a) Tambua na ueleze aina ya shairi hili. (alama 1)
b) Fafanua ujumbe katika shairi hili. (alama 5)
c) Tambua bahari za shairi kwa kuzingatia vigezo ulizopewa. (alama 2)
   i) vipande
   ii) vina
d) Fafanua mbinu alizotumia mshairi ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 4)
e) Tambua toni ya shairi hili. (alama 1)
f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari. (alama 4)
g) Tambua maana ya misamiati kama ilivyotumiwa katika shairi. (alama 3)
   i) tafrani
   ii) anahanja
   iii) kubazazi

***<u>7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.</u>***

**M. Nyanje: Si Kitu**

Sinongi aushi yangu, hii leo, kwa ukungu wa ujana,
Nikaiga rika langu, kwa vileo, na mbio za wasichana,
Kiwa ni riziki yangu, mapokeo, kuoa na kuoana,
Ni wakati utanena.

Nashukuru kwa ugumba, wenye ndimi, wanipagazao nao,
Wapitao wakiimba, eti mimi ningapenda hali zao,
Haupandiki mgomba, wana nyemi, risadi wa hadhi zao,
Eti ni kwa raha zao.

Ni lipi lenye kukera, kwa muumbi, marufuku kwenye misa,
Ni mtu kuwa hawara, wa vitimbi, ama alozawa tasa?
Ugumba na ukapera, sio dhambi, wala haujawa kosa,
Waama sina makosa.

Bora tungeni vitabu, magazeti, mutangaze kwa rediyo,
Muwaite watribu, kina siti, watuzwa ilimu hiyo,
Na zaidi muhutubu, kwa umati, muwambe ambayo siyo,
Kwalo sichafuki moyo.

KIELELEZI SAHIHI

Hidhuru yote ni bure, sio kitu, kudhiki asodhikika,
Siwi nikaona ghere, lailatu, nyota njema itafika,
Kwa shangwe na njerejere, kila mtu, mdomo utafumuka,
Akiri amejibika.

***(Mwalaa M.Nyanje)***

a. Uleza **ujumbe wa shairi** hili (alama 4)
b. Fafanua kwa kutoa mifano, mbinu nne alizotumia mshairi **kutosheleza mahitaji yake ya kiarudhi** katika shairi hili. (alama 8)
c. Nafsineni (mzungumzaji) katika shairi hili inasema na pande mbili. Zieleze pande hizo. (alama 2)
d. Eleza **umuhimu wa maswali ya balagha** katika shairi hili. (alama 3)
e. Bainisha **toni** ya shairi hili. (alama 1)

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

**8 Soma kifungu kisha uyajibu maswali**

**Mzee mkuu:** *(akiwa ameshika fimbo)* Wanakijiji, ukame umetutesa sana. Mashamba yamekauka na mifugo inaangamia.

**Mama:** ni kweli mzee. Watoto wanalia kwa njaa kila siku.

*(wanakijiji wanakusanyika na kuleta maziwa, asali na mbuzi)*

**Mzee Mkuu:** *(huku akiinua mikono juu)* Ee mizimu ya mababu, tupeni mvua na Baraka. Ondoeni mateso katikakijiji chetu.

*(gafla radi inasikika mbali)*

**Wanakijiji:** amina! Amina!

Mzee Mkuu: Tazameni! Mawingu yanaanza kukusanyika!

Wanakijiji: (kwa furaha) Mvua! Mvua inakuja!

a) Eleza kipera hiki. (alama 2)
b) Eleza shughuli tatu zinazohushishwa na kipera hiki. (alama 3)
c) Fafanua umuhimu wa kipera hiki katika jamii. (alama 6)
d) Eleza matayarisho yanayofaa kufanywa kabla ya kuanza shughuliza ukusanyaji data wa kipera hiki nyanjani. (alama 5)
e) Eleza umuhimu wa mtambaji wa fasihi simulizi kushirikisha hadhira katika uwasilishaji wake. (alama 3)

KILELEKEZI SAHIHI

# KIELEKEZI 3

**SEHEMU YA A: USHAIRI.**

***1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Leo kitaka nifike, natamani, ila wauma mwili
Kwa kazi nihusike, samahani, unahiliki mwili
Napenda nihesabike, makundini, ila huwezi mwili.

Vitisho pamwe kelele, ninavicha, kwa nafsi na mwili
Ili ugonjwa utimile, umechacha, na kuudhili mwili
Msikose simile, magalacha, si gurudumu mwili

Vingekuwapo viraka, kuutia, ngeusuguruti, mwili
Kifundi kivipachika, kuingia hata kuridhi mwili
Upya ukaungulika, kuvutia, roho na wake mwili

Lakini kamwe haiwi, kuvipata, vipande vyake mwili
Sihofu kupata mawi, sitajuta, kupigania mwili
Hata kufutwa sikawi, nitakita, kidete nao mwili

Kazi ninaithamini, ni hakika, akilini na mwili
Ila kamwe siamini, kusagika damu, jasho na mwili
Uwele hususani, kioneka, nguvu hitishi mwili

a. Eleza **dhamira ya mtunzi** wa shairi hili. (alama 4)
b. Fafanua **mbinu nne za lugha** zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 8)
c. Eleza **toni ya shairi** hili. (alama 2)
d. Ni nani **anayezungumziwa na nafsineni** katika shairi hili. (alama 1)
e. Eleza **bahari ya shairi** hili kwa kurejelea vipande. (alama 2)
f. Andika ubeti wa mwisho katika **lugha ya nathari**. (alama 3)

KIELEKEZI SAHIHI

## SEHEMU B: RIWAYA

**Clara Momanyi:** *Nguu za Jadi*

*Jibu swali la 2 au la 3*

**2. "<u>Chombo chao sasa kimepanda mwamba</u>. Mizengwe yao sasa imewatumbukia nyongo."**

i. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

ii. Mbinu za lugha zinazopatikana katika dondoo. (alama 2)

iii. Thibitisha ukweli wa maneno ya dondoo hili. (alama 14)

**3. "Eh!... simamisha gari. Yule mwanamke lazima akamatwe. Ndiye aliyetaka kuniangamiza wakati mmoja!"**

i. Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

ii. Eleza umuhimu wa anayerejelewa na msemaji. (alama 6)

iii. Eleza mikakati ya Lonare kuhakikisha kuwa amekabiliana na njama za Lesulia katika harakati zake za kupigania jamii yake. (alama 10)

## SEHEMU C: TAMTHLIA

**Timothy M. Arege:** *Bembea ya Maisha* *Jibu swali la 4 au la 5*

***<u>4. Soma kifungu kisha uyajibu maswali</u>***

**Madaktari wameeleza chanzo cha maradhi yako hayo. Ndoa imeyatia doa maisha yako. Imekuletea msongo wa mawazo kwa kukaripiwa na hata kupigwa na baba. Sasa mimi ninataka uhuru wangu na sitataka kupigwa kichapo cha mbwa mara kwa mara mpaka nipate ugonjwa wa moyo. Matokeo yake ni haya. Kuna raha gani kama maisha ni kugeuzwa ngoma ukapigwa kwa fujo yote mpaka ukapasuka?**

a) Fafanua <u>umuhimu wa mbinu za kitamathali</u> zilizotumika katika dondoo. (alama 4)

b) Eleza maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

c) Onyesha jinsi mwandishi alivyofanikiwa kutumia mbinu ya jazanda ukirejelea tamthlia ya Bembea ya Maisha. (alama 12)

KIELELEZA SAHIHI

**5. "Maradhi!.. Dawa zikiingilia huku, maradhi hutokezea pale hali pesa zinakwenda, shughuli sinasimama. Mifuko hufukarika lakini zaidi huleta wasiwasi usioisha. Ningekuwa na uwezo ningefanya chochote madhali ugonjwa uondoke. Dunia ina mitihani tosha lakini panapo maradhi sugu, uzito wake hauamithiliki. Inabaki kumwomba Mola afanye wepesi huku ukijipigapiga kutafuta jawabu."**

i. Changanua mtindo katika nukuu (alama 5)

ii. Eleza umuhimu wa mandhari katika nukuu. (alama 6)

*iii.* Eleza jinsi Asasi ya ndoa ilivyosawiriwa katika tamthlia ya *Bembea ya Maisha.* *(alama 9)*

## SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

**D.W Lutomia na Phibian Muthama:** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

**Jibu swali la 6 au la 7**

**6. Alimwona kama mtu mwingine na hakuamini. Siku zote walizoishi alimpenda mkewe. Aliamini hajaona mwanamke mwenye bidii kama huyu. Kwa bidii alifanya ulezi na uzito wote wa ndoa uonekane kanda la usufi. Hata yeye Adan alihisi alipoingia nyumbani matatizo yaliyokuwa yakimsumbua yameingia katika kaburi la sahau na basi hapo hakuzinga huku wala kule. Alijua kuwa kama mkewe alitaka kusoma, lazima asimame naya kwa hali na mali mpaka atimize ndoto yake.**

a) Tambua mbinu za kimtindo katika kifungu hiki. (alama 4)

b) Eleza maudhui yanayojitokeza katika kifungu. (alama 6)

c) Fafanua changamoto za watoto mayatima kulingana na hadhithi ya Toba ya Kalia. (alama 10)

7. **"Matusi yaliyoje? Mwanamke anamwambia mumewe kuwa ni mzembe!"**

**a)** Eleza muktadha wa maneneo haya. (alama 4)

**b)** Jadili maudhui ya ubabedume jinsi yanavyojitokeza katika hadithi ya Nipe Nafasi. (alama 12)

**c)** Bainisha vikwazo vikuu kwa maendeleo ya wanawake ukirejelea hadithi ya Nipe Nafasi. **(alama 6)**

KIELELEZO SAHIHI

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

***8. Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali***

Mtambaji alijibwaga ulingoni kuwasilisha kipera chenye sifa zifuatazo;

*Mhusika alikuwa shujaa mwenye uwezo mkubwa usio wa kawaida.*

*Mhusika alikuwa daima anawindwa na maadui.*

*Hatimae mhusika aliangamizwa kwa kupuuza jambo ndogotu.*

i. Tambua kipera chenye sifa hizo. (alama 2)
ii. Eleza umuhimu wa kipera hiki katika jamii. (alama 6)
iii. Eleza umuhimu wa nyimbo katika uwasilishaji wa fasihi simulizi. (alama 6)
iv. Fafanua mbinu tano za sasa za kukusanya fasihi simulizi. (alama 6)

KIELEKEZI SAHIHI

# KIELEKEZI 4

## SEHEMU A: RIWAYA

**Clara Momanyi:** *Nguu za Jadi*

**1. "Daktari amesema tusijaribu kusema naye maana moyo wake umedhoofika sana."**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. (alama 6)

c) Eleza jinsi mandhari tofauti tofauti yanavyowakuza wahusika mbalimbali(alama 10)

## SEHEMU B: TAMTHLIA

**Timothy M. Arege:** *Bembea ya Maisha*

*Jibu swali la 2 au la 3*

**2. "Hiyo ndiyo ajabu! Kizazi hiki hakitaki kufanya kazi. Kinataka kuja kazini kwa sababu ya mshahara tu. Wachapa kazi hodari ni jozi iliyopotea. Nilipokuwa na afya yangu tulishirikiana kutafuta riziki ya kuwalea hawa watoto wetu. Kweli japo mara nyingi haikuwa rahisi tulijitolea hadi tukashinda. Leo hali ni tofauti na bila yeye na moyo wake rahimu wa kusaidia, sijui wenzake wangekuwaje. Wasichana wengi wakiolewa husahau ndugu zao. Hutupa jongoo na mti wake. Sisi tuna bahati ya mtende…"**

a) Changanua mtindo katika kifungu hiki. (alama 4)

b) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

c) Eleza maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

d) Kila mwanajamii anafaa kushiriki katika kumkomboa mwanamke. Thibitisha kwa kurejelea tamthlia nzima. (alama 8)

**3. Jadili jinsi suala la utu limeshughulikiwa na wahusika wanawake katika tamthlia ya *Bembea ya Maisha.*** (alama 20)

KIELEKEZI SAHIHI

## SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

**D.W Lutomia na Phibian Muthama:** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4. "...naomba unipeleke mjini japo sina hela, kwa bahati mbaya nimepoteza kipochi changu. Nisaidie kakangu."**

a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b) Eleza sifa za msemaji zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)
c) Eleza jinsi tamaa iliyokidhiri aliyokuwanayo msemaji wa maneno haya
d) ilivyomtumbukiza kwenye lindi la kutamauka. (alama 6)
e) Eleza umuhimu wa mandhari ya mgodini kwa mujibu wa hadithi ya Mapambazuko ya Machweo. (alama 6)

**5. "Ingawa nimefikia magharibi ya maisha yangu, sudi hii imenipa tumaini la mapambazuko mapya maishani. Nahisi kwamba jua la asubuhi limeangazia miale ya matumaini mapya…"**

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Eleza toni inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 1)
c) Eleza mbinu mbili za kimtindo zinazojito keza katika dondoo. (alama 2)
d) Eleza mambo yanayozuia miale ya matumaini mapya kwa wengi ukirejelea hadithi ya Mapambazuko ya Machweo. (alama 13)

KIELEKEZI SAHIHI

## SEHEMU YA D: USHAIRI

*Jibu swali la 6 au la 7*

***6. Amiri A.S Andanenga; sauti ya kiza***

Ngakua na mato, ya kuonea
Ngalisana kito, cha kuchezea
Kilicho kizito, cha kuelea
Kikamuenea, akivae.

Makusudi yangu, ngaliandaa
Ngamfanyanga chungu, cha mduwaa
Ngatia vitangu, vinavong'aa
Ili ziwe taa, kwa apikae

Mkungu wa tano, wa mduwara
Ulo bora mno, kisha imara
Ulo na maono, kuwa ni dira
Kwenye barabara, itandae.

Ngaomba Baraka, kwake Rabana
Punji za nafaka, kila aina
Chunguni kuweka, kwa kulingana
Hajaangu suna, yule alae.

Ngafanya bidii, kwenda mwituni
Sio kutalii kukata kuni
Ya miti mitii huko jikoni
Isiyo na kani ni iwakae

Kwangu mabega, nikathubutu
Ngabeba maiiga, yalo matatu
Simba tembo chatu, sinitishie.

Miti yenye pindi, na jema umbo
Ngajenga ulindi, mwema wimbombo
Fundi aso fundi, penye kiwambo
Moyo wenye tarabo, apekechae

Singaajiri, ngachimba mi mi
Kizima kizuri, cha chemchemi
Maji ya fahari, ya uzizimi
Jua la ukami, siyaishae

Tamati nafunga, kwa kuishia
Mato ndo malenga, kanikimbia
Nahofu kutunga, mabeti mia
Asije chukia, ayasomae

**2014**

a. Eleza **ujumbe** wa shairi hili. (alama 2)
b. Kwa kurejelea ubeti wa pili **eleza umuhimu wa aina mbili za idhini** alizotumia mshairi. (alama 4)
c. Andika ubeti wa saba kwa **lugha ya nathari**. (alama 4)
d. Eleza **toni** ya shairi hili. (alama 2)

KIELEKEZI SAHIHI

e. Fafanua **aina tatu za urudiaji** zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 6)
f. Bainisha **nafsineni** katika shairi hili. (alama 2)

***<u>7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.</u>***

Nalilia mazingira yetu haya
Hakuna kilicho safi
Vyote ni kombo
Mrama vimekwenda

Tazama mto huo
Mto utambao katikati mwa jiji kuu
Jiji la uzungu na usasa
Lenye warembo na wakwasi
Wanaolivuna bila fahamu
Wanaolilima bila kujali
Wanalifumbia macho ilhali lipo!

Najua mwakani watakuja usafi kulitia
Usafi ndugu wa siku moja
Eti kuupa mji sura!
Wanaukosha mji, si mto!

Ni mto ulioona mengi na makubwa kushuhudia
Lakini kwa kimya ndugu zangu unakwenda
Labda kwa uchovu na bughudha
Ningekuwa mimi ningepaaza sauti:
"Punguzeni bughudha. Msinitwike mizigo yenu

Maana mimi mnanibebesha mizigo yenu
Na minyororo ya uchafu kunitia
Kusudi mpate safika. Tangu lini
Mtu kukoshwa kwa sabuni? Hamjui
Mto husafisha dhambi?"

Lakini nionavyo ndugu
Taswira ya mto huu
Ni taswira kamilifu ya kizazi chetu!
Kizazi baina ya kilichopita na kijacho.

KIELELEZA SAHIHI

(**Limenukuliwa Kutoka:** *Tunu ya Ushairi*)

a) Eleza ujumbe wa shairi hili. (alama 5)
b) Onyesha mbinu **mbili** za uhuru wa kishairi katika shairi hili. (alama 2)
c) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. (alama 3)
   i. Tashihisi
   ii. Swali la balagha
   iii. Kinaya
d) Onyesha **aina mbili za urudiaji** zinazojitokeza katika ubet wa pili. (alama 2)
e) Bainisha **nafsineni** katika shairi hili. (alama 1)
f) Fafanua **aina tatu** za taswira kwa kurejelea shairi hili. (alama 3)
g) Eleza **toni** ya shairi hili. (alama 2)
h) Andika **ubeti wa tatu** katika lugha ya nathari. (alama 2)

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

***8. Soma utungo ufuatao kisha uyajibu maswali;***

**Tangu siku hiyo, kuku ameishi kuchakura ardhini akitafuta wembe wa mwewe.**

a) Tambua kipera hiki. (alama 1)
b) Eleza umuhimu wa fomula ya mwisho wa hadithi. (alama 4)
c) Fafanua mbinu tano za kisasa za kukusanya fasihi simulizi. (alama 5)
d) Eleza faida zinazoandamana na uhifadhi wa fasihi simulizi kupitia kwa mbinu za kisasa. (alama 4)
e) Jinsi hadhira itakavyochangia katika utambaji wa hadithi. (alama 6)

KIELELEZI SAHIHI

## KIELEKEZI 5

**LAZIMA- FASIHI**

***1. Soma utungo huu kisha uyajibu maswali yafuatayo;***

**Mfumbaji** : Nina fumbo, je mtalifumbua?
**Wafumbiwa** : Ndio tutalifumbua
**Mfumbaji** : Fatuma ana vitu vitatu; paka kuku na unga anataka kuvusha mto. Paka hula kuku na kuku hula unga. Kulingana na kanuni za kuvuka daraja lile, huwezi kuvuka ukiwa na zaidi ya vitu viwili. Je fatuma atatumia njia gani ili avuke?
**Wafumbiwa** : kwanza atavusha paka na unga kisha atarudi na kumchukua kuku
**Mfumbaji** : Sahihi, amepata

**Maswali**

(a) Tambua utanzu wa kipera hiki. (alama 1)
(b) Eleze sifa za kipera zinazojitokeza katika utungo. (alama 4)
(c) Eleza utaratibu maalum wa uwasilishaji wa mafumbo. (alama 4)
(d) Eleza umuhimu wa kipera hiki katika maisha ya vijana wa sku hizi. (alama 4)
(e) Tambua tofauti zilizopo kati ya mafumbo na vitendawili. (alama 3)
(f) Eleza faida za kutazama uwasilishaji wa kipera jukwaani kuliko kusoma vitabuni. (alama 4)

### SEHEMU B: RIWAYA

**Clara Momanyi:** *Nguu za Jadi*

*Jibu swali la 2 au la 3*

**2. "Tumefanya zote, mama. Lakini kuna swali moja la *business* ambalo lilinishinda,"**

i. Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
ii. Eleza umuhimu wa msemaji wa maneno haya. (alama 6)
iii. Mwanamke ni mhimiri mkuu katika kujenga jamii. Huku ukirejelea riwaya ya Nguu za Jadi, thibitisha ukweli wa kauli hii (alama 10)

**3. "Jimbi leo keshawika. Alidhani akimfungia pakachani hatawika? Hamna siri duniani mwanangu..."**

i. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
ii. Eleza sifa za msemaji wa maneno haya. (alama 5)
iii. Onyesha jinsi mwandishi alivyotumia mbinu ya sadfa katika uwasilishaji wake. (alama 11)

KIELEKEZI SAHIHI

## SEHEMU C: TAMTHLIA

**Timothy M. Arege:** *Bembea ya Maisha Jibu swali la 4 au la 5*

**4. "Maisha ni haya uyaonayo ya kujituma kama kitoto kidogo. Ukiamka ng'ombe anakusubiri zizini akitaka apelekwe malishoni. Kuku nao ndio hao kinyesi kila mahali- kinakutaka upangusepanguse na kufagia. Jiko linakungoja uliwashe na kujiandalia chochote utie kinywani, na baada ya kufungua kinywa vyombo navyo vinakusubiri uvitie maji. Bado nazo kazi za shamba zinakungoja. Hata ukiwapa watu vibarua bado inakuhitaji uwe pale uwalinde kutwa nzima kama askari jela. Lau sivyo utakuta wamekupunguzia kile kidogo ulichowaita kuja kukitengeneza."**

i. Changanua mtindo katika kifungu hiki. (alama 5)

ii. Eleza maudhui manne yanayojitokeza katika kifunguMaudhui. (alama 4)

iii. Eleza Jinsi Yona anavyoendeleza mbinu ya kinaya. (alama 11)

iv.

**5. "Hivi ndivyo walivyofanya wazee wetu. Mavuno ya kwanza huonjwa na wazee na kutoa Baraka"**

i) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

ii) Eleza jinsi maudhui ya ubabe dume yanavyojitokeza ukirejelea tamthlia ya Bembea ya Maisha. (alama 10)

iii)Eleza mchango wa msemaji wa maneno haya katika kuendeleza ploti ya tamthlia. (alama 6)

## SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

**D.W Lutomia na Phibian Muthama:** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

**Jibu swali la 6 au la 7**

**6. "*Okay*," nilisema kabla ya kuendelea, "Unajua mwisho wa mwezi ni kesho tu. Halafu… eeh… kidogo anasema hali imemlemea. Anaomba kama kampuni inaweza kumpa advansi ya shilingi elfu tano hivi ili aweze kulipia kodi ya nyumba. *Landlord* anatishia kumfungia nyumba kwa sababu anadhani Nilakosi anataka kumlaghai."**

a) Changanua mtindo katika kifungu. (alama 4)

b) Onyesha jinsi wahusika katika hadithi ya *Harubu ya Maisha* walivyopata harubu ya maisha. (alama 9)

c) Eleza umuhimu wa matumizi ya dayalojia katika hadithi hii. (alama 7)



KIELELEZI SAHIHI

**7. "Kisa cha mke wa Suluhu kilikuwa kama msumari moto kwenye kidonda kibichi"**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Eleza sifa za mke wa Suluhu. **(alama 4)**

c) Eleza Umuhimu wa mwandishi kutumia mbinurejeshi **(alama 12)**

## SEHEMU YA D: USHAIRI

*Jibu swali la 8 au la 9*

8. Ushaona

Nchi kupiga hatua bila Amani?
Unajua mazao ya kitali?
Unajua hofu inayowapatta wanachi
Vita kutamalaki nchi mwao
Ushawahi kujisaili kuhusu kiini cha adharusi
Ushawahi kujiuliza ni kina nani huchochea vita hivyo?
Wanavipalilia ili mali wendelee **kuhodhi**
Na kujitwalia mamlaka

Vinapotokea ni nani huumia?
Bila shaka si wakata wanokatika
Ajabu hino ajabu
Wanyonge kupigania wakwasi wongeze mali
Makatili mabepari wawacheka wanyonge
Wakichinjwa ja wanyama
Wakata wakijifia huombolezwa kwa sekunde
Damu yao kiunda mto
Haya yote wachochezi, runingani hutazama!

Hofu nayo huwangia
Wanyonge wanyongwao
Kazi zao hawafanyi
Kihofia mavamizi
Njaa nayo huwakumba
Wengi wao kujifia
Mainzi nayo hwicheka miili yao kwa sauti
Ugomvi huwangia walopendana awali

Mali ilo ya thamani
Huharibiwa kwa sekunde

KIELEKEZI SAHIHI

Unaona madhara yake?
Vita lozaliwa na wachochezi
Walotaka kutawala?
Kumekucha!
Kataeni ada hii!
Kwokoa nti yetu kwahitaji nao utu
Utu kutoka kwa wanyonge na walo na mali tele
Nch kupinga hatua ni juhudi zao wote.

a) Jadili madhara ya hali inayozungumziwa na mshairi. (alama 5)
b) Fafanua mbinu tatu za kimtindo katika shairi hili. (alama 3)
c) Fafanua aina mbili za urudiaji katika shairi hili. (alama 2)
d) Onyesha matumizi mawili ya mishata katika shairi hili. (alama 2)
e) Fafanua mbinu alizotumia mshairi ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)
f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari. (alama 4)
g) Tambua toni katika shairi hili. (alama 1)

***9. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali yafuatayo***

Ningali kinda nishike, viungo vi teketeke,
Sinipe simi nizuke, na vichaka nivifyeke,
Dhibiti nivuvumke, usidiriki makekeke,
Pilika usikiuke, mpe mtoto hakiye,

Mungavunja haki yake, madhara milele kwake
Wa kiume na wa kike, mpeni yaliyo yake,
Kwa makini mumshike, kadiri makamo yake,
Pulika msikiuke, mpe watoto haki,

Kwanza ni watani wake, uandae aridhike
Atunze mtima wake, maudhi yasimshike,
Kuta nne zizunguke, na hofu imbaduke,

KIELEKEZI SAHIHI

Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake

Pili ni chakula chake,'jengeke siha yake'
Mpe titi alishike, anyonye asihinike,
Kuta nne zizunguke, na hofu imbanduke,
Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake

Mpe tiba 'sidhurike, ndwele asiathirike
Fikira zimpanuke, atambue rika lake
Penye daraja avuke, mvushe asighurike,
Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake

Angakuwa chekecheke, apande shule avuke
Mpe taaluma yake, adhibiti apanuke,
Ufundi na nidhima zake, ayashike ajivike,
Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake

Jifanye kipenzi chake, mpende asihinike
Amani ijae kwake, daima isikereke
Vizito usimtikwe, visivyo vipimo vyake
Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake

Elimu chuo ishuke, apanuke bongo lake
Atende jukumu lake, ahudumie wenzake
Ajue wajibu wake, atende asitepweke

KIELEKEZI SAHIHI

Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake

Hima kwa Muumba wake, muhimidi aongoke

Roho yake isafike, ahera isisumbuke

Neema imzunguke, maovu yamuepuke

Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake

**MASWALI**

a) Nafsi neni ametaja haki zinazomstahiki mtoto. Zitaje na uzifafanue (alama 4)

b) Eleza kwa kutoa mifano mbinu mbili zinazotumiwa na mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi (alama 4)

c) Bainisha umuhimu wa tamathali zozote mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili (alama 4)

d) Eleza ubeti wa tano kwa lugha nathari (alama 4)

e) Taja na ufafanue toni ya mshairi (alama 4)

f) Eleza maana ya msamiati ifuatayo (alama 2)

i. Mtima

ii. Asihinike

iii. Mbi

iv. Asighurike

KIELEKEZI SAHIHI

# KIELELEKEZI 6

## SEHEMU A: TAMTHLIA

**Timothy M. Arege:** *Bembea ya Maisha*

**1. "Niache nicheke mama. Hii *servant quarter* inanitosha. Kwanza mtaa huu si kila mtu anayeweza kuishi. Chumba hiki kinaonekana kidogo lakini kodi yake ni sawa na inayolipiwa nyumba ya vyumba viwili katika mitaa mingine. Kijijini nitarudi na elimu yote niliyopata? Watu watashangaa."**

i. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

ii. Eleza mbinu za lugha zinazojitokeza katika dondoo. (alama 4)

iii. Eleza matatizo ya kuishi mjini kama yanavyojitokeza katika tamthlia ya Bembea ya maisha. (alama 12)

## SEHEMU B: RIWAYA

**Clara Momanyi:** ***Nguu za Jadi***

*Jibu swali la 2 au la 3*

**2. "Wanawake mna umbea na unaa nyie. Vidhabi wa Taria. Hata hamwachi tupumzike mkashughulikie yenu. <u>Bure yenu hiyo</u>!**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Eleza umuhimu wa nidaa katika dondoo (alama 1)

c) Eleza umuhimu wa msemji katika dondoo kwa mujibu wa mandhari haya. (alama 8 )

d) Eleza kinaya kinachojitokeza katika maneno yaliyopigwa mstari katika dondoo. (alama 7)

**3. "Kwenda! Waketwa ni watu wasio na akili hata ya kuchagua wachumba. Ndio maana daima mnabaki nyuma kama makoti. Hata sijui kwa nini nilikuajiri."**

i. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

ii. Eleza maudhui matatu yanayojitokeza katika dondoo. (alama 3)

iii. Eleza toni tatu zinazojitokeza katika dondoo. (alama 3)

iv. Eleza madhira yaliyowapata Waketwa. (alama 10)

KIELELEKEZI SAHIHI

## SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

**D.W Lutomia na Phibian Muthama:** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4. "Umejibaidi nami kama ardhi na mbingu na sasa sina budi kusema nawe kwa njia hii ya barua kwa kuwa kitumbua kimeingia mchanga."**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza nafsi iliyotumika katika dondoo. **(alama 1)**
c) Eleza mbinu za kisanaa zilizotumika katika dondoo. **(alama 3)**
d) Eleza ukweli wa maneno yaliyopigiwa mstari kwa kurejelea hadithi nzima ya Kifo cha Suluhu. **(alama 13)**

5. Eleza jinsi maudhui ya ajira inavyojitokeza katika hadithi ya Mapambazuko ya Machweo.

(alama 20)

## SEHEMU D: USHAIRI

**JIBU SWALI LA 6 AU LA 7**

**6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Naingia ukumbini, nyote kuwakariria,
Ushairi niwapeni, hoja nitawaachia,
Mnipe masikioni, shike nachoeleza,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

Naanza kwa uzalendo, nchi yetu tuipende,
Yadhihirishe matendo, nchi yetu tuipende,
Wa kila mtu mwendo, usije kawa mpinde,
Taifa sio taifa, pasi kuwa na maadili,

Linda demokrasia, uongozi tushiriki,
Haki kujielezea, wachotaka na hutaki,
Changu naweza tetea, demokrasia haki,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

KIELELEZA SAHIHI

Tuwe na uadilifu, twache tamaa na hongo,
Tusiwe na udhaifu,wa kuwa watu waongo,
Tukomeshe uhalifu, kisha tuache maringo,
Taifa sio taifa, pasi kuwa na maadili,

Ubinafsi si adili, ila ni kusaidia,
Ukiwa nayo mali, asiye nacho patia,
Kama mtu mswahili, ubinafsi mtu achia,
Taifa sio taifa, pasi kuwa na maadili,

Na inavyoelezea, katiba ni kielezi,
Tutii kwa mazoea,hadi kijacho kizazi
Kwa hayo nitamwachia hiyo ya ziada kazi,
Taifa sio taifa, pasi kuwa maadili.

a) Eleza mambo yoyote **manne** ambayo mshairi anashauri taifa lifanye ili kuwa na maadili.(alama 4)

b) Eleza mbinu za kimtindo zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)

c) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: (alama 2)
i) Mpangilio wa vina
ii)Vipande katika mshororo.

d) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

e) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)

f) Eleza umuhimu wa aina **mbili** za uhuru wa mshairi zilizotumiwa katika ubeti wa nne. (alama 4)

g) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama 4)

**AU**

***7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Nakuusiya mwanangu, na waovu jihadhari,
Haswa mpika majungu, ajifanyao mzuri,
Kumbe moyowe ukungu, umezagaa wa shani,
Fuma rafiki wa kheri, usijepata matungu.

Pambanua walimwengu, siyo wote wenye kheri,
Kuna watu ni vipungu, wenye midomo khatwari,
Tabasamu lao fungu, mbeleyo na neno zuri,
Ni alo kwako johari, akupigao marungu.

KIELEKEZI SAHIHI

Mchague kwa vifungu, rafiki yako vizuri,
Ni yule mwenye utungu, la shari likikujiri,
Hufurahi mlimwengu, furahani ukiswiri,
Hukupa na ushauri, mwema ujazao nyungu.

Hakukimbii ja nungu, dhiki zikikudawiri,
Husimama ja mkungu, nawe akiwa ngangari,
Kukufinika na wingu, la sitara kusitiri,
Hapo ndipo hudhihiri, kilicho kwenye mvungu.

Kumbata wasiya wangu, ujana una ghururi,
Mtague mwenye pingu, mawi anaejibari,
Ambae ni mcha Mungu, mwenye tele tabaswuri,
Jitenge naye jeuri, hufunzwa na ulimwengu.

Natinda kauli yangu, hapano kwenye shairi,
Tambua ewe mwanangu, rafiki mwema uturi,
Alomui hawi dungu, ni moshi wake tanuri,
Asiyavyoge hadhari, maji yenye nyungu nyungu.

***Maswali***

(a) Fafanua ujumbe wa mshairi. (alama 4)
(b) Bainisha bahari katika shairi hili. (alama 3)
(c) Bainisha vipengele vya kimtindo vinavyojitokeza kwenye ubeti wa kwanza. (alama 3)
(d) Bainisha toni ya shairi hili. (alama 1)
(e) Onyesha mbinu alizotumia mshairi kutimiza mahitaji ya kiarudhi. (alama 2)
(f) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 4)
(g) Eleza umbo la shairi hili. (alama 3)

KIENYEKEZI SAHIHI

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

**8. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

*Nililitizama jua la kinjano*
*Likijikokota kwa jitimai kutua*
*Mbele ya nguu*
*Ya mlima uso kikomo*
*Likipisha machweo*
*Yenye giza la kaniki*
*Likishindilia uzito wa nanga*
*Kwenye moyo tepetevu*
*Uloonja shubiri ya kwondokewa.*

*Twalitazamana na hiyo shamsi*
*Ikipotelea kwenye upeo wa macho*
*Huku nyuma ikinambia*
*"Yamekwisha."*
*Niliona kope zake zikimezwa na kiza*
*Nikaliona jua likitoweka pamwe nawe*
*Jagina wa maisha yangu*
*Nikaliona likikokota aushiyo*
*Likabwakura rohoyo*
*Kutoka kwenye vyangu vitanga*

*Kumbukizi zilikuleta*
*Kwenye jukwaa la akili yangu*
*Pazia likafunguka*
*Likayaleta mawio*
*Ya siku ya kuamkia kuuka kwako*
*Nilikuona kwenye ruya ikitazamana ana kwa ana*
*Na hasidi alokakawana*
*Kutuhasiri mi nawe*
*Nilikiona kipaji chako*
*Kikitwaa wasiwasi*
*Ukawa ni kama wanywea*
*Kwa wake mtazamo.*

KIELEKEZI SAHIHI

*Hata uliponishika*
*Mkono kunambia*
*Tukimbile tujiponye*
*Nalikuwa nimechelewa*
*Ulikuwa keshanipa kisogo, huku*
*nyuma waniita,*
*"mwanangu, njoo tujisalimishe*
*Mwanangu njoo, nguvu zimenisha."*
*Kumbe hiyo ilikuwa tahadhari*
*Kwamba izraili yu karibu*
*Moyowe kuchukua?*
*Kumbe wali ukisema, "Buriani mwanangu?"*

*Siku ya faradhi ilifika, mkono kulazimika kukupungia*
*Niliutazama mwilio mtukufu*
*Nililitazama tambolo liloumbika*
*Wali umedhibitiwa shujaa wangu*
*Ndani ya chumba chenye kuta*
*Na paa la mbao*
*Hata tulipokukaribisha,*
*Kwa lako kaburi*
*Nilijipa kujiambia, "Hajenda popote*
*Mtima bado wapiga."*
*Nalingoja unisalimu*
*Nalingojea tabasamu lako lenye haya*
*Ela hayo hayakutimila*
*Walikuwa kesha kwenda*
*Kuwa milki, ya ardhi isoshiba.*

*Hata waliponena, "Udongo kwa udongo,"*
*Nilikusikia ewe yeli uso kifani*
*Ukighani ubeti wa wimbo*
*Wako pendwa mawazoni mwangu*
*"Kifo ni hasidi,*
*Ikiwa mimi gunge*

KIELELEZI SAHIHI

*Roho yangu nitamkabidhi Iziraili*
*Mimi niliyekaidi bunduki ya Mzungu*
*Katika kitali cha miaka minne*
*Kwetu kikarudi fahari na jina*
*Mimi niliyeshindana na ndui na tetekuwanga, iliyowapukutisha*
*Wana wote wa ngome*
*Nikabaki mimi, jogoo wa kijiji.*

*"Kifo ni shujaa,*
*Ikiwa mimi Gunge mwili wangu huu mtukufu*
*Kwa tambo na nemsi*
*Nitaukubalia*
*Kuwa lengo la dua za kuonewa Imani*
*Kwa karamu ya macho ya mahasimu*
*Kuvikwa suti na mwosha*
*Kufunikwa kwa udongo uliolaaniwa*
*Mimi Gunge,*
*Niliruhusu jabali kubwa*
*Likibinye changu kichwa*
*Likidhibiti changu kidari*
*Linizibe zangu pumzi*
*Gunge niache kutawala."*

**Maswali**

(a) Huu ni wimbo wa aina gani?
(b) Andika sababu mbili kuthibitisha jibu lako hapo juu.
(c) Nani anayeimbiwa na nafsineni?
(d) Bainisha matatizo mawili yanayoikumba jamii inayosawiriwa na utungo huu.
(e) Eleza Sifa za wimbo aina hii
(f) Eleza majukumu ya mbolezi
(g) Bainisha mbinu zifuatazo katika wimbo huu;
  i. Ritifaa
  ii. Mbinu rejeshi
  iii. Taashira
(h) Unanuia kutumia mbinu ya kutazama na kushiriki kufanya utafiti kuhusu nyimbo za aina hii. Eleza sababu sita za kuchagua mbinu hii.
(i) Wewe ni mwasilishaji wa kipera cha wimbo jukwaani, eleza mambo ambayo utazingatia katika uwasilishaji wako
(j) Eleza toni inayojitokeza katika wimbo huu.

KIELEKEZI SAHIHI

# KIELELEKEZI 7

**SEHEMU YA A- LAZIMA**
**SHAIRI**

**1. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Ulimwengu ulimwengu, ulimwengu naratibu
Yaliyo kichwani mwangu, nataka kuyahutubu
Wayasome ndu zangu, wa mbali na wa karibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ulimwengu ni kiwanja, cha wenye raha na tabu
Wengine wanajikonja, kwa wengine ni adhabu
Kucha na kutwa twahanja, kutafuta matulubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa balaa, aliniusia babu
Mna mambo yamejaa, ya faraja na kusibu
Na machache ya kufaa, ila mengi ya udubu
Cha weye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja cha Amina, Saidi Ali Rajabu.
Wengine kitu hatuna, tunaishia kababu
Wale wamejaza sana, wanashindwa kuhesabu
Cha wenye raha na tabu, Ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa urongo, na kweli pia ajabu
Kichwa hudanganya shingo, tumbo kiuno chasibu
Usitumai ubongo, wa nduguyo na swahibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa walevi, pombe kwao ni dhahabu

KIELEKEZI SAHIHI

Mara vile mara hivi, wakilewa majudhubu
Maneno ya kiujuvi, hujipaka hata shabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja wenye dini, wamtiio wahabu
Mashekhe msikitini, humo humfanya muhibu
Mapadiri kanisani, huvihubiri vitabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja

Ni uwanja wa malofa, lofa mtu mwenye tabu
Kusema sana kashifa, na moyo kisebusebu
Tunakaribia kuja, kwa kushidwa kujimudu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa faraja, alowajali habibu
Na wengine sitotaja, msinambe ninagubu
Ni uwanja wa viroja, vigumu kuvikutubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

***Maswali:***

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama.1)

(b) Eleza umuhimu wa idhini ya mshairi ulivyotumika katika shairi. (alama.4)

(c) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. (alama.4)

(d) Taja na ueleze mikondo katika shairi hili. (alama.3)

(e) Fafanua sura ya shairi hili. (alama.4)

(f) Tambua na uthibitishe toni ya shairi hili. (alama.2)

(g) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi. (alama.2)

KIELEKEZI SAHIHI

## SEHEMU B: RIWAYA

## Clara Momanyi: *Nguu za Jadi*

*Jibu swali la 2 au la 3*

**2. "*This can't be…how*? Siku zote hizi nimekuwa nikimtusi yule mzee. Ati ni baba yangu? Siamini mpaka nimwone."**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Taja mbinu mbili za lugha ambazo zinajitokeza katika dondoo. (alama 2)
c) Eleza nafasi ya mwanamke katika jamii ya wamatuo (alama 12)

**3. Jadili mbinu walizotumia Wakule kuendeleza uongozi wao dhalimu. Al 20**

## SEHEMU C: RIWAYA

## Timothy M. Arege: *Bembea ya Maisha*

*Jibu swali la 4 au la 5*

**4. "Nikipata Bunju wangu si nitakuwa nikilia mpaka niende hospitalini kuongezewa machozi?"**

i. Eleza muktadha wa maneno haya (alama 4)
ii. Eleza mbinu za lugha zinazojitokeza katika dondoo. (alama 2)
iii. Tambua toni inayojitokeza katika dondoo. (alama 1)
iv. Eleza umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. (alama 7)
v. Sara ametumiwa na mwandishi kufuna maadili. Thibitisha ukirejelea tamthlia ya Bembea ya Maisha. (alama 6)

**5. "Sijui mbona huelewi! Siku zote nimekuambia kimasomaso tena kwa lugha ya wazi kuhusu hili. Wajibu wangu nitafanya na nimejitolea kutekeleza kwa hali na mali kufikia hapo. Wewe unajua uzito wa majukumu niliyo nayo."**

i. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
ii. Fafanua mbinu mbili za kimtindo ambazo zinajitokezakatika dondoo. (alama 2)
iii. Eleza umuhimu wa msemaji wa maneno haya. (alama 6)
iv. Eleza umuhimu wa mnenewa wa maneno haya katika kuendeleza maudhui. (alama 8)

KIELELEZI SAHIHI

## SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

**D.W Lutomia na Phibian Muthama:** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

**Jibu swali la 6 au la 7**

**6. "Kiokote usiye na shukrani wewe! Mjalaana mkubwa! Huogopi kunitajia kuwa umeanza kupokea barua za kijinga! Leo utarudi kwa huyo mwanamume anayekudanganya kuwa umekua…baradhuli mkubwa wee… utanitambua!"**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Eleza tamathali za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

c) Eleza toni inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 1)

d) Eleza matatizo amabayo watu wa jinsia ya mnenewa wanayopitia. (alama 11)

**7. "Ondoa wasiwasi mhibaka, *you are in very safe hands*. Usiulize maswali, its *okay*. Tulikuja sote jana baada ya *dance*, umesahau hivi?**

b) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

c) Eleza mbinu za kisanaa zinazojitokeza katika dondoo. (alama 2)

d) Thibitisha kuwa mwandishi amefanikiwa kutumia mbinu rejeshi katika hadithi ya Kila Mchezea Wembe. (alama 14)

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

***8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali***

Fanani 1 (Wambua): Wazee wazee eee!

Hadhira: eee!

Fanani 1: Wazee wazee aaa!

Hadhira: Aaa!

Fanani 1: Mnaona Otis, Kichwa chake ni kipara hadi nzi akisimama anaslide!

Fanani 2 (Otis): Wazee wazee eee!

Hadhira: eee!

Fanani 2: Wazee wazee aaa!

Hadhira: Aaa!

Fanani 2: mnaona Wambua, ni mweusi hivi kwamba ukiingia kwa nyumba watu hufikiria usiku umeingia.

**Maswali**

(a) Tambua kipera hiki cha mazungumzo. (alama 1)

(b) Eleza sifa za kipera hiki. (alama 5)

(c) Kipera hiki kina umuhimu gani katika jamii. (alama 5)

(d) Eleza sababu za utani wa kale kufifia. (alama 4)

(e) Eleza hasara tano za miviga. (alama 5)

KILEKWA SAHIHI

## KIELEKEZI 8

### SEHEMU YA A: HADITHI FUPI

**D.W Lutomia na Phibian Muthama:** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

**1. Aligutuka kwenye usingizi wa mang'amung'amu, roho mkononi, pumzi zikimwenda mbio. Hakujua kilichomwamsha, hivyo alitega sikio ndi! Isije ikawa mwenye nyumba kaja na yeye mpangaji akachelewa kumfungulia mlango; itakuwa balaa bin belua. Ndio maana amelala pale juu ya kochi ili akiingia tu, hata kabla ya kubisha mlango, awe tayari kuufungua. Hilo litampa usalama japo kwa muda tu. Baada ya kusikiliza kwa makini na kuchungulia nje, hakumwona aliyemtarajia. Asaa akaamua asifike leo.**

a) Eleza muktadha wa maneno ya dondoo hili. (alama 4)
b) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 6)
c) Eleza maudhui matatu yanayojitokeza katika dondoo hili. (alama 3)
d) Suala la umaskini limejitokeza katika hadithi "Pupa" Thibitisha. (alama 7)

### SEHEMU B: RIWAYA

**Clara Momanyi:** ***Nguu za Jadi***

*Jibu swali la 2 au la 3*

2. **Katika siku za hivi karibuni, Mangwasha alikuwa akimfikiria mumewe sana. Baada ya kwenda uhamishoni Chakani, alirudia tena maisha ya ulevi. Mwishowe alifutwa kazi na mkewe hakujua aliko. Lakini lililomtia huzuni ni kwamba wanawe sasa walikuwa wamemsahau. Hawaulizi yuko wapi, sebuse kumtaja! Aidha aliwaza na kuwazua kauli za Sagilu kuhusu mumewe.**

a) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 3)
b) Eleza maudhui manne yanayojitokeza katika kifungu. (alama 4)
c) Thibitisha kuwa, "Hakuna marefu yasiyokuwa na ncha."ukirejelea riwaya nzima. (alama 13)

**3. "Kuna waliomwita mnyakuzi huku wengine wakimwita dudumizi kwani alinyemelea viota vya wengine. Hajengi bali hubomoa"**

i. Eleza muktadha wa dondoo hii. (alama 4)
ii. Tambua mtindo katika dondoo hili (alama 4)
iii. Onyesha jinsi mrejerelewa alikuwa hajengi bali hubomoa. (alama 10)



KIELEKEZI SAHIHI

## SEHEMU C: TAMTHLIA

**Timothy M. Arege:** *Bembea ya Maisha*

*Jibu swali la 4 au la 5*

**4. "Kazi ikawa nikuwasema; wakalaumiwa na kusutwa. Watu wakanong'ona na kusema faraghani. Haikuwa rahisi kwao..."**

a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b) Eleza sifa za anayezungumziwa katika dondoo hili. (alama 6)
c) Fafanua mbinuishi wanazotumia wahusika mbalimbali kukabiliana na changamoto wanazopitia kwa kurejelea Bembea ya Maisha. (alama 10)

**5. "Maana magari mengi ni kachara tu. Unadhani umepanda gari kumbe kebe la mabati yaliyoungwa na kupakwa rangi. Mara nyingi sisi abiria hupanda rangi badala ya gari."**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Fafanua mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo. (alama 2)
c) Eleza umuhimu wa msemewa wa maneno haya katika kuendelezaploti ya tamthlia ya Bembea ya Maisha (alama 14)

**SEHEMU YA D: USHAIRI.**

**Jibu swali la 6 au 7**

***6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Nakuja jamani, muanga kuwatolea,
Kwani ninayo Imani, ni wengi wamepotea,
Kwa hiyo nawaombeni, niruhusu kwongea
Elimu nawambieni, kwamba haina kikomo.

Elimu yawatolea, mwajua ni kitu gani,
Elimu ikipokea, utakuwa thawabuni,
Kitu gani nasemea, fikirini jijibuni
Elimu nawambieni, kwamba haina kikomo.

Kaya unapoachia, unaingia shuleni
Jama mkifikiria, kweli huko ni kazini,
Hesabuni waingia, na kusoma nyingi fani,
Elimu nawambieni, kwamba haina kikomo.

KIELEKEZI SAHIHI

Tangu ukiwa nyumbani, elimu unaanzia,
Kule kunawa usoni, nalo somo angalia
Kuna mafunzo jandoni, na huko kumbini pia
Elimu nawambieni, kwamba haina kikomo.

Unapotoka shuleni, ulimwenguni wangia,
usipofunzwa nyumbani, utafunzwa na dunia,
Je humo elimuni? Jaribu kuniambia
Elimu nawambieni, kwamba haina kikomo.

Kwimba nako kizoea, jela ni kwako nyumbani
Maisha hukuzoea, si tabu ni kitu gani?
Hayo sijayakosea, kama soi somo semeni
Elimu nawambieni, kwamba haina kikomo.

Hatakuwa na fitina, ukiwa safi rohoni,
Hutathaminika sana, uwapo wa kurubuni,
Nambieni la maana, siyo elimu jamani?
Elimu nawambieni, kwamba haina kikomo.

Ujiweke ulevini, tabuni waogelea,
Na ukiwa ugenini, yafaa nini ongea,
na ukiwa ugenini, soni hutajionea?
Elimu nawambieni, kwamba haina kikomo.

Niwapo ufukarani, mawazo hunifuata
Wapi nitie mpini, cha tumboni kukipata,
Hapo nimo mafunzoni, uvivu nini waleta
Elimu nawambieni, kwamba haina kikomo.

Mambo mengi mumepata, kwa hiyo angalieni,
Karibuni kuyafata, muyatie akilini
La maana hukupata, usitie maanani
Elimu nawambieni, kwamba haina kikomo.
***(D.P.B. Massamba)***

(a) Fafanua kwa hoja sita mtazamo wa nafsineni kuhusu elimu kwa mujibu wa shairi hili. (alama 6)
(b) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika ubeti wa tano. (alama 2)
   i. Tanakuzi

KILIMANJARO SAHIHI

ii. Tashihisi

(c) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)

(d) Fafanua mbinu mbili ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi kutoka ubeti wa sita hadi wa kumi (alama 4)

(e) Bainisha toni katika shairi hili (alama 2)

(f) Andika ubeti wa kwanza katika lugha ya nathari. (alama 2)

**J. Kiponda: Mwanangu Sikubali**

***7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Mwanangu, wenye dhambi vishawishi, vikejeli
Mwanangu, katu wasikushawishi, bilikuli
Mwanangu, aushi nayo uishi, kama mwali
Mwanangu sikubali

Mwanangu, washerati sikuperembe, kakubali
Mwanangu, usiwache wakubembe, kwa Sali
Mwanangu, mithili yao mapembe, ya fahali
Mwanangu sikubali

Mwanangu, wajeuri siwe nao, ni shubili
Mwanangu, usifwate njia zao, pita mbali
Mwanangu, ujeuri sera yao, mazohali
Mwanangu sikubali

Mwanangu, waongo usiwasifu, kulihali
Mwanangu, uongo ubatilifu, si amali
Mwanangu, ndimi zao hazikifu
Mwanangu sikubali

Mwanangu, wafisadi siwe nao, kemikali
Mwanangu, tamaa ndo utu wao, si Injili
Mwanangu, wahepe kila uchao, kiakili
Mwanangu sikubali

Mwanangu, wote walio wabaya, wanadhili
Mwanangu, usije ukawapeya, ikibali
Mwanangu, katika hino duniya, kaa mbali
Mwanangu sikubali

KIELEKEZI SAHIHI

a) Fafanua **mambo sita** ambayo yanaweza kuzorotesha maadili ya anayelengwa na shairi hili. (alama 6)
b) Bainisha **tamathali mbili za usemi** zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
c) Andika **aina mbili za urudiaji** zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
d) **Ainisha shairi** hili ukizingatia vigezo vifuatavvyo: (alama 4)
   i. Idadi ya vipande katika kila mshororo.
   ii. Mpangilio wa maneno katika kila mshororo
   iii. Idadi ya mizani katika mishororo
   iv. Mpangilio wa vina katika kila ubeti.
e) Andika aina mbili za **idhini ya kishairi** zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
f) Andika ubeti wa tano katika **lugha ya nathari**. (alama 4)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

***8. Soma kifungu kisha ujibu maswali***

**Vijana *tibim*! Wazee hoiyee! Na Madem *Mwaaah*! Jambo moja ninapenda ya wakale ni kuwa Mkale hata akiwa na njaa umwulize kama amekula atakwambia *bato*.**

a) Tambua utanzu wa kifungu hiki. (alama 2)
b) Ufanisi wa uwasilishaji wa utanzu huu unategemea fanani. Thibitisha (alama 5)
c) Eleza jinsi jamii ya kisasa inavyoendeleza kipera hiki. (alama 6)
d) Eleza umuhimu wa kushiriki moja kwa moja unapofanya utafiti wa kipera hiki. (alama 4)
e) Eleza sababu za kudidimia kwa ngomezi katika jamii ya kisasa. (alama 3)

KIELEKEZI SAHIHI

## KIELEKEZI 9

### SEHEMU A: RIWAYA
### Clara Momanyi: *Nguu za Jadi*

**"Ama kweli, elimu ni maisha si vitabu"**

a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

b) Eleza umuhimu wa muzungumzaji wa maneno haya. **(alama 5)**

c) Fafanua jinsi asasi ya ndoa ilivyosawiriwa ukirejelea riwaya nzima. **(alama 11)**

### SEHEMU B: TAMTHLIA
### Timothy M. Arege: *Bembea ya Maisha*

*Jibu swali la 2 au la 3*

**2. "Lazima nimshukuru kwa vitendo kwa jinsi alivyojitolea kuijenga familia yetu. Kwaheri pombe. Buriani."**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Eleza mbinu moja inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 1)

c) Tambua toni inayojitokeza katika dondoo (alama 4)

d) Eleza umuhimu wa uzungumzi nafsia wa Yona kuhusu ulevi wake na afya ya mke wake (alama 8)

e) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili (alama 6)

**3. "Pamoja na kero zake za mara kwa mara, nilijua kuwa watoto si nguo za kutungua."**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Eleza maana ya sitiari iliyotumika katika dondoo. **(alama 4)**

c) Eleza sifa za msemaji wa maneno haya (alama 4)

KIELEKEZI SAHIHI

## SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

**D.W Lutomia na Phibian Muthama:** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4. "Maisha ya wanamatopeni yalikuwa kama mchezo wa karata, hawajui leo wala kesho!"**

a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

b) Onyesha kwa ufafanuzi jinsi uongozi mbaya unavyojitokeza katika hadithi ya Msiba wa Kujitakia. (alama 16)

5. **"Amina… wallahi nafa njaa! Tafadhali nisaidie. Ikibidi nipe hata kibarua nifanye. Nitafanya tu bora jamaa yangu ipate chakula…hata cha leo tu…"**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Eleza umuhimu wa nidaa katika dondoo. (alama 1)

c) Eleza mbinu wanazotumia viongozi kuingia mamlakani katika nchi ya Matopeni. (alama 15)

**Kilio cha lugha**

***<u>6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali</u>***

Ni wimbo najiimbia, nijiliwaze
Sina wa kusaidia, **nasongwa** sina nafasi
Kiwa kwetu naumia, kwengine sio mahususi
Lugha ya mtu mweusi, Kiswahili chalilia

Wataalamu ni nani, mulipo mwaninyanyasa
Hamna nami imani, wala kupanga siasa
Mwasema sayansini, siku ningalitosa
Mwanambia nikotosa, kuiva sijafika

Ela muelewe sana, Maamuna na Imamu
Mlipokuwa vijana, kwenu nilikuwa timamu
Sasa mumesoma sana, mwaniona ni haramu
Mujue kuwa dawamu, utumwa mwauridhia

Mzaliwapo mwalia, 'maa', maneno ya kwanza
Lugha munayokulia, ya mama zetu ya kwanza
Wa lugha muwedoria, muweze na kuikuza
Sio kujipendekeza, uzungu kuigiza

KIELEKEZI SAHIHI

Majira ya ukoloni, ukombozi kusambaza
Lugha mulithamini, Kiswahili kufukiza
Hata kule risavuni, kizungu hanikuwaza
Sasa mbona mwanibeza, mbali mwanitupilia?

Sayansi sio asili, msamiatiwe sinao
Sayansi yataka mbali, msamiati ni wa hao
Nitakuwa Kiswahili, kiomba majina yao
Lugha kujikuza kwao, huomba linalifaa

Enyi viongozi wetu ipangeni nadharia
Kujenga siasa yetu, tuzidi kuwa huria
Lugha hata 'mbusha' watu, tuche **kuriaria**
Sifa ni kwa chake mtu, cha mwenzi hutoringia

Utajiri wangu hasa, nikiwatajia wote
Msamiati huwa, ni wa Afrika yote
Na methali za kuasa, nahau na ngeli zote
Na nisemwapo popote, ujumbe hukamilika

Afrika ndipo petu, pa wabantu halisi
Baba na mama ni Bantu, sina la wangu ukwasi
Warabu na wengi wetu, sio wangu **adinasi**
Kwao 'meomba kiasi ili kujizidisha.

Mfumo mpya hongera, wa elimu humu Kenya,
Lugha takuwa imara, ukabila tutafinya
Kiswahili ni ibara, kila mtu kiimanya
Methali imetuonya, mtumwa si mwasalia

Tamati lugha yalia, yabaguliwa bayana
Kukua imeridhia, msamiati kufana
Wengine wataijulia, kwa marefu na mapana
Lugha yenu ya maana, mwaipuuza yalia

a. Shairi hili ni la **aina gani**? Toa sababu. (alama 2)
b. Kwa kutoa hoja nne, eleza kwa nini shairi hili likaitwa kilio cha lugha. (alama 4)
c. Andika ubeti wa tatu kwa **lugha ya nathari**. (alama 4)
d. Eleza **toni ya shairi** hili. (alama 2)


KITUI EKEZI SAHIHI

e. Tambua **uhuru wa kishairi** uliotumiwa kwa kurejelea mifano mitatu. (alama 3)
f. Bainisha **nafsineni** katika shairi. (alama 2)
g. Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mujibu wa shairi. (alama 3)
   i. Nasongwa
   ii. Kuriaria
   iii. Adinasi

***7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Nimeyaandika maneno haya
Kwa niaba ya:
Mamilioni wasio malazi
Wabebao vifurushi vilivyo wazi
Wazungukao barabarani bila mavazi
…milki yao ya maisha
Kwa niaba ya:
Maelfu wanaouawa bila haki
Wiki baada ya wiki
Leo sumu au spaki
Leo Kamba au bunduki
Na kwa wale wanosubiri kunyongwa.

Kwa niaba ya:
Vijana walio mitaani
Wale mayatima wa maskini
Wazungukao mapipani kila
pembe mjini
kuokota sumu kutia tumboni
kujiua bila kujua
ili kupata kuishi.
Kwa niaba ya:
wakongwe wasio jiweza
walao chakula kilichooza
wachukuao choo wakijipakaza
pole pole wakijiangamiza
katika vyumba vyao
baridi na giza
kwa sababu hawana
watazama wala wauguza

KILEKEZI SAHIHI

kwa niaba ya:
waishi na nyingi hofu
kwa sababu ya madawa tifutifu
yatiwayo vyakulani yakitufanya wafu
bila ya mtu kuona
kama kwamba sote tu vipovu

na kwa niaba yetu sote:
tuliofungwa vifungoni, duniani
tuliosukumwa kingoni, maishani
tuliopokonywa maoni, machoni
tuliotiliwa sumu, malishoni
tuliodidimizwa kinyesini
ili 'maendeleo'
yaendelee kwenda njiani
huku yakitema machicha ya roho zetu.

a) "Shairi hili linakatisha tamaa" thibitisha kauli hii kwa kutoa **mifano saba** kutoka kwenye shairi. (alama 7)
b) Fafanua **umuhimu wa aina mbili za urudiaji** zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 4)
c) Bainisha **vipengele** vifuatavyo **vya kimtindo** katika shairi hili. (alama 3)
   i. Tasfida
   ii. Kinaya
   iii. Tashihisi
d) Eeza kwa kutoa mfano, mbinu moja ambayo mshairi ametumia **kutosheleza mahitaji ya kiarudhi** katika ubeti wa tano. (alama 2)
e) Andika ubeti wa pili katika **lugha ya nathari**. (alama 2)
f) Bainisha **nafsineni** katika shairi hili. (alama 2)

KILIFEKEZI SAHIHI

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

***8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali***

Hapo zamani za kale Maulana aliitazama dunia na akaamua kuwatuma wajumbe wawili. Wajumbe hawa wakawa ni Kinyonga na Chiriku. Wa kwanza kutumwa alikuwa kinyonga ambaye alipewa ujumbe kuwa mwanadamu hata aga dunia. Kinyonga aling'oa nanga na kuteremka kwa mwendo wa kuduwaa, akisimama kila mahali alipoona matunda na kuyambugia. Hivyo basi kinyonga alichelewa kuufikisha ujumbe kwa mwanadamu. Mungu alipoona hivyo aliamua kumtuma chiriku na ujumbe kwamba mwanadamu sharti afariki dunia. Chiriku alipeperuka haraka kama umeme na akawahi dunia kabla ya kinyonga kufika. Mara moja akatangaza ujumbe "Wanadamu sharti kufa!" na akarejea kwa Mungu bila kubananga wakati. Hatimaye kinyonga akafika duniani na kutangaza "Wanadamu hamtafariki!" wanadamu wakapinga na kusema, "La hasha! Tumeshaa pata ujumbe wa chiriku mwanadamu sharti kufa! Hatuwezi kupokea tena neno lako! Basi kutokana na neno la Chiriku wanadamu hufa.

**Maswali**

(a) Eleza na uthibitishe kipera hiki. (alama 2)

(b) Eleza mbinu za kisanaa zinazopatikana katika hadithi hii. (alama 3)

(c) Hadithi hii ina umuhimu gani. (alama 5)

(d) Eleza sifa za visasili. (alama 6)

KIELEKEZI SAHIHI

## KIELEKEZI 10

### SEHEMU YA A: LAZIMA
### TAMTHLIA *BEMBEA YA MAISHA*

**1. Mami, mbona wacheka peke yako? Aaah, acha nicheke mwanangu.**

i. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

ii. Fafanua madhira yanayompata anayecheka peke yake. (alama 6)

iii. Matatizo yanayowakumba wanamatuo ni mwiba wa kujidunga. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea Nguu za Jadi. (alama **10)**

### SEHEMU B: RIWAYA
### Clara Momanyi: *Nguu za Jadi*

*Jibu swali la 2 au la 3*

2 a) **"Subiri kwanza. Wajua, mila hairuhusu mke kumfuata mumewe kwenye starehe zake."**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Huku ukirejele Riwaya ya Nguu za Jadi, bainisha nguu mbalimbali zilizotinga maendeleo ya nchi ya Matuo. (alama 10)

c) Matatizo yanayowakumba wanamatuo ni ya kujiletea wao wenyewe. Thibitisha huku ukirejelea riwaya yote (alama 10)

b) Vijana wamekumbwa na changamoto chungu nzima. Thibitisha kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi. (alama 10)

### SEHEMU YA C: HADITHI FUPI
### D.W Lutomia na Phibian Muthama: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4. "Mume wako? Nikiwa hapa mimi ni gavana si mumeo. Pigia mhazili wangu simu mfahamishe."**

a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

b) Fafanua sifa za muzungumzaji wa maneno haya. (alama 4)

c) Eleza mbinu mbili za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

d) Eleza toni inayojitokeza katika dondoo. (alama 1)

e) Maudhui ya ukatili yamejitokeza kwa mapana katika hadithi ya Fadhila za Punda. Thibitisha ukweli wa kauli hii. (alama 9)

KIELEKEZI SAHIHI

**5. "Hawajui hawa. Nitapata mwandani kama mke wangu marehemu? Hatoshi yeyote yule kujaza pengo aliloliacha mke wangu mpenzi."**

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

**b)** Eleza mambo yanayowatia wahusika tofautitofauti wasiwasi katika hadithi ya Fadhila za Punda. (alama 10)

**c)** Eleza ufaafu wa anwani, Fadhila za Punda (alama10)

## SEHEMU YA D: SHAIRI

Jibu swali 7 au 8

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Nieleze
Ewe binadamu mwenza
Ni mara ngapi
Uzungumzapo na jirani?

Utembelewapo na ninga
Wakachanganyika na kuku
Kwenye ua la nyumba
Huku kwa midomo ya kasi
Wakidondoa punje na punje
Unawauliza hali yao
Au magharibi ipigapo hodi
Unawatazama wakirudi makwao
Bila neno la uchunguzi
Kutoka kinywani?

Wewe wa ukoo wangu
Umewahi kuuliza mkwaju
Mkwaju, hebu nambie
Nijapo kwako kila mwaka
Na kuvijaza vikapu kwaju
Pasipo chembe ya mbolea
Wala kopo la maji
Unaniona jirani mwema
Au adui wa kuchukiwa?

Usimamapo kando ya njia
Ama kwenye mbalamwezi inayozagaa
Nyota zinazometemeta
Au jua linalong'ara

KIDUKEZI SAHIHI

Na kupakua kibofu
Juu ya tosi za miche
Macho ya maua
Au mapafu ya mtambazi
Umewahi kusema:
    Nambieni
    Mnaonaje tabia yangu,
    Ni ya mwenza muungwana
    Au jirani mtundu?

Uamkapo asubui na mapema
Ukaanza mwendo wa kwenda shamba
Kuinga kima, tumbili na nyani
Wasidhuru mahindi au mtama
Na njiani
Ukakuta na kifa-uongo mkongwe
Kwa kuema na machovu
Akisukuma tonge la shonde
Unamwamkua kwa heshima
Au unampuuza na kumpita?

Anga ya usiku nakawa ingiapo
Ikapendeza kwa pambo linalometemeta
Unaanzisha mazungumzo na nyota
Unapekua mienendo ya mbingu za mbali
Unadadisi sayari, miezi na vimwondo
Au hiyo elimu isiyokera kwa karo
Unaipuuza kwa ujeuri
Na kubakia katika giza?
***(Kithaka wa Mberia: Nieleze – Bara Jingine)***

**MASWALI**

a) Fafanua ujumbe wa shairi hili. (alama 5)
b) Tambua nafsineni katika shairi hili. (alama 2)
c) Andika mifano miwili ya mistari mishata katika shairi hili. (alama 2)
d) Fafanua aina mbili za taswira kwakurejelea shairi hili. (alama 2)
e) Andika mifano ya mbinu zifuatazo za kimtindo kwenye shairi. (alama 3)
   i. Uradidi
   ii. Uhuishi
   iii. Ritifaa
f) Fafanua toni katika shairi hili. (alama 2)
g) Andika ubeti wa tatu katika lugha ya nathari.
(alama 4)

KIELEKEZI SAHIHI

***8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

U wapi ujana wangu, na madhubuti ya nia?
Niko hapa peke yangu, ujana umepotea
Umeanacha na machungu, mambo niliyozoea
Kuwa na uwezo wangu, nayo imeshika njia,
Siku za ujana wangu, nazo sizioni pia,
Nadhari sasa si yangu, tazama hii dunia!

U wapi ujana wangu, ubingwa na mazoea?
Ndugu za jamaa zangu, na watu niliojua,
Wamehama ulimwengu, ni pweke nimebakia
Nguvu wanazo wenzangu, sasa wanazitumia
Nikishikacho si changu, ajabu hii dunia.
Hutia kizunguzungu, wakati wa kuchungua
Kama hukumbuki Mungu, kufuruni utakuwa

U wapi ujana wangu, na maringo ya tabia?
Hamna kinywani mwangu, jino lililobakia,
Na laini gumu kwangu, sina cha kutafunia
Kitamu sasa kichungu, hata kama ni halua
Kama ningefungwa pingu, sina la kufurahia
Katika maisha yangu, nimebaki na fadhaa
Kama fumbo ulimwengu, na watu wazuzuliwa.
***(S. Robert)***

a. Bainisha kwa **hoja tano** kinyume kinavyojitokeza katika shairi hili. (alama 5)
b. Eleza **muundo wa shairi** hili. (alama 4)
c. Eleza **aina nne za taswira** katika shairi hili. (alama 4)
d. Onyesha mifano ya **mbinu** zifuatazo katika shairi hili. (alama 4)
   i. Kweli kinzani
   ii. Tashihisi
   iii. Tasfida
   iv. Usambamba
e. Bainisha **nafsineni** katika shairi hili. (alama 1)
f. Eleza **toni** ya shairi hili. (alama 1)

KIELEKEZI SAHIHI

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

***8. Soma kifungu kisha ujibu maswali***

**Cha mkufuu mwanafu ha na aki hu. Cha mwanafu mkufu hu na aki ha.**

a) Tambua kipera hiki ni kipi . (alama 1)

b) Eleza umuhimu wa utanzu huu katika jamii. (alama 6)

c) Ili kudumisha utanzu wa semi, jamii inaweza. (alama 5)

d) Umuhimu wa kukusanya na kuhifadhi habari kuhusu fasihi simulizi. (alama 5)

e) Maandishi ni mojawapo ya vifaa vya kukusanya na kuhifadhi fasihi simulizi. Tathmini udhaifu wa kutumia kifaa hiki. (alama 3)

**ZIADA**

***8. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayouata***

**Dhamiri yangu**

Dhamiri imenifunga shingoni.
Nami kama mbuzi nimefungwa
Kwenye mti wa utu. Kamba ni fupi
Na nimekwishachora duara.
Majani niwezayo kufikia yote nimekula.
Ninaona majani mengi mbele yangu
Lakini siwezi kuyafikia: kamba, kamba

Oh! Nimeungwa kama mbwa.
Nami kwa mbaya bahati, katika,
Uhuru kupigania, sahani ya mbingu,
Nimeipiga teke, na niigusapo kwa mdomo,
Mbali saidi inakwenda na siwezi tena
Kuifikia na hapa nilipofungwa
Nimekwishachafua na kuhama siwezi

Kamba isiyoonekana haikatiki.
Nami sasa sitaki ikatike, maana,
Mbuzi wa kamba alipofunguliwa, mashambani,
Aliharibu na mbwa aliuma watu
Ninamshukuru aliyenifunga hapa,
Lakini lazima nitamke kwa nguvu
"Hapa nilipo sina uhuru!"

(E.Kezilahabi)

KIHEKEZI SAHIHI

**Maswali**

a) Taja mambo manne ambayo mshairi analalamikia. (alama 4)
b) Kwa nini mshairi haoni haja ya yeye kuwa huru? (alama 2)
c) Eleza maana ya mshororo ufuatao kama ilivyotumika katika shairi. "kamba isiyoonekana haikatiki'' (alama 2)
d) Eleza **mbinu za kimtindo** zinazojitokeza. (alama 2)
e) Taja na utoe mifano miwili, eleza jinsi **matumizi ya mishata** yanavyojitokeza katika shairi hili. (alama 4)
f) Andika ubeti wa pili kwa **lugha nathari**. (alama 4)

KIELEKEZI SAHIHI